

UCHANGANUZI WA MAKOSA YA KIFONOLOJIA YANAYOFANYWA
NA WAZUNGUMZAJI WA KIKAMBA WANAPOJIFUNZA KISWAHILI
SANIFU

NA

MBULA J. EDWARD

University of NAIROBI Library



0532187 2

Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya M.A.
katika Chuo Kikuu cha Nairobi

2011

UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa kwa mahitaji ya shahada katika Chuo kikuu kingine chochote.



18/11/2011

MBULA J. EDWARD

TAREHE

(MTAHINIWA)

Tsanifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu tukiwa wasimamizi wa kazi hii wa Chuo Kikuu cha Nairobi



21/11/2011

DKT. IRIBE MWANGI

TAREHE

(MSIMAMIZI)



21/11/2011

DKT. NYACHAE MICHIRA

TAREHE

(MSIMAMIZI)

TABARUKU

Tasnifu hii naitabarukia wanangu wapendwa Henry Wambua, Edward Musyoki na David Mutuku pamoja na marafiki wangu wa karibu wakiwemo Daniel Mutuku, Collins Mwema walionihimiza kila mara safari iliponiwia ngumu. Vilevile, naitabarukia wazazi wangu wapendwa Edward Mutune na Rebecca Mutune walionilea na kunifunza thamani ya mtoto wa kike kupata elimu na kujitegemea. “Mama; Mungu akupe maisha marefu ili uone matunda ya kazi na bidii yako”.

SHUKRANI

Mwanzo kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai na uwezo wa kutimiza ndoto yangu ya kupata shahada ya uzamili katika somo la Kiswahili. Nawashukuru wahadhiri wote wa idara ya isimu na lugha za Kiafrika kwa mchango wao kupitia ushauri walionipa.

Shukrani zangu za dhati nazitoa kwa wasimamizi wangu Dkt. Iribemwangi na Dkt. Nyachae Michira na pia wahadhiri wote walionisaidia kwa mawazo, wakiwemo Prof. Habwe, Dkt. Ayubu Mukhwana, Dkt. Zaja Omboga, Dkt. Kineene wa Mutiso na Prof. Wamitila.

Nawashukuru wanafunzi wenzangu ambao tuliableti pamoja katika jahazi moja na kuhakikisha tumefika mwisho licha ya mawimbi mengi. Nao ni Nyaga, Watua, Karinge, Murage, Apopo, Mwanjala, Mohanda, Kinywa, Amos, Angela, Kitali na wengine.

Nawashukuru marafiki zangu Simbiri, Langat, Njuguna, Dajom na Luvayo kwa upendo wao na pia kunihimiza nisikate tamaa maishani. Nawashukuru ndugu zangu Nicholas Mutune na Collins Mwema kwa kuwa ndugu wema waliofurahi nami kila mara nilipopiga hatua maishani.

Nawashukuru dada zangu Lynnex Vaati, Ann Ndunge na Sheila Wavinya walionihimiza katika safari hii. Kwenu wote mlioshiriki kufanikisha kazi hii nasema asante.

YALIYOMO

| | |
|--|------|
| Ungamo | ii |
| Tabaruku | iii |
| Shukrani | iv |
| Yaliyomo | v |
| maelezo ya Dhana Zilizotumiwa | viii |
| Orodha ya istilahi na ishara zilizotumiwa..... | ix |
| Mukhtasari | x |

SURA YA KWANZA

| | |
|---|----|
| 1.1 Utangulizi..... | 1 |
| 1.2. Tatizo la Utafiti..... | 2 |
| 1.3. Madhumuni ya utafiti..... | 4 |
| 1.4. Nadharia tete | 5 |
| 1.5. Sababu za kushughulikia tatizo..... | 5 |
| 1.6. Upeo na mipaka ya utafiti..... | 6 |
| 1.7. Yaliyoandikwa kuhusu tatizo hili | 6 |
| 1.8. Msingi wa nadharia..... | 12 |
| 1.9. Njia za utafiti | 15 |

SURA YA PILI

FONIMU ZA KISWAHILI SANIFU NA KIKAMBA

| | |
|---|----|
| 2.1. Sifa bainifu na uanishaji wa fonimu za Kiswahili Sanifu..... | 17 |
| 2.2. Sifa bainifu na uainishaji wa fonimu za Kikamba..... | 18 |
| 2.2.1 Fonimu za konsonanti za Kiswahili sanifu | 18 |
| 2.2.2 Irabu za Kiswahili sanifu | 26 |

| | |
|--|----|
| 2.3 Fonimu za Kikamba, sifa bainifu na uainishaji | 28 |
| 2.3.1 Konsonanti | 29 |
| 2.4 Uainishaji wa Irabu | 28 |
| Hitimisho | 36 |
| SURA YA TATU | |
| MUUNDO WA SILABI KATIKA LUGHA YA KISWAHILI SANIFU NA KIKAMBA | |
| 3.0. Utangulizi..... | 38 |
| 3.1. Muundo wa silabi katika lugha ya Kiswahili..... | 39 |
| 3.2. Muundo wa silabi katika Kikamba | 42 |
| 3.3. Ulinganishi Na Ulinganuzi Wa Miundo Ya Silabi Za Kiswahili Na Kikamba | 47 |
| 3.3.1. Ulinganishi wa miundo ya silabi za Kiswahili na Kikamba | 48 |
| 3.3.2. Ulinganuzi wa miundo wa silabi za kikamba na Kiswahili | 51 |
| Hitimisho | 52 |
| SURA YA NNE | |
| UCHANGANUZI WA MAKOSA KWA MISINGI YA NADHARIA | |
| 4.0 Utangulizi..... | 53 |
| 4.1 Mifano ya makosa yanayofanywa katika kila mihimili | 54 |
| 4.2 Uchanganuzi | 59 |
| SURA YA TANO | |
| MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO | |
| 5.1 Utangulizi | 60 |
| 5.2 Muhtasari | 60 |
| 5.3 Hitimisho | 61 |

| | |
|-----------------------|----|
| 5.4 Mapendekezo | 64 |
| Marejeleo | 65 |
| Kiambatisho | 67 |

MAELEZO YA DHANA ZILIZOTUMIWA

- LUGHA - KATI - Ni lugha inayojitokeza wakati mwanafunzi anapo jifuza lugha ya pili. Lugha hii huwa imekiuka kanuni za lugha lengwa hivi kwamba hujitokeza kama lugha kamili yenye mfumo wake wa kiiisimu.
- LUGHA YA KWANZA - Hii ni lugha ambayo mtoto hujifunza mara ya kwanza anapozaliwa. Pia hurejelewa kama lugha asilia au lugha ya mama. Ni msingi wa lugha hii ambapo lugha ya pili hujengeka.
- LUGHA YA PILI - Ni lugha ambayo mtu hujifunza baada ya kujifunza lugha yake ya kwanza. Hii ni lugha ambayo watu wengi hujifunza katika masomo.

ORODHA YA ISHARA ZILIZOTUMIWA

| | | |
|---------|---|------------------|
| L1 | - | Lugha ya Kwanza |
| L2 | - | Lugha ya pili |
| K | - | Konsonanti |
| I | - | Irabu |
| Kons | - | Konsonanti |
| Kip | - | Kipasuo |
| Naz | - | nazali |
| Kiy | - | kiyeyusho |
| Kit | - | kitambaza |
| Kim | - | kimadende |
| // | - | Fonimu |
| Kik | - | kikwamizwa |
| Kiz-kik | - | kizuiwa kwamizwa |
| Sil | - | silabi |
| \$ | - | mpaka wa silabi |

MUHTASARI

Utafiti huu unanuia kuchanganua makosa ya kifonolojia yanayofanywa na wazungumzaji wa kikamba kama lugha ya kwanza wanapoijifunza Kiswahili sanifu kama lugha yao ya pili. Ili kufikia malengo, utafiti huu umetumia nadharia ya lugha - kati kama ilivyopendekezwa na Selinker (1972) hasa mifanyiko yake mitano ya kisaikolojia. Hivyo ilibidi tupange kazi hii kwa sura tano kama ifuatayo.

Sura ya kwanza imeshughulikia utangulizi, tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, nadharia tete, sababu za kuchagua mada hii, upeo na mipaka ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada hii, msingi wa kinadharia na njia za utafiti.

Katika sura ya pili, tumeshughulikia, uainishaji wa fonimu za Kiswahili sanifu pamoja na fonimu za Kikamba. Hapo ndipo tumebainisha sifa bainifu za fonimu mbalimbali pamoja na kuangazia. Katika sura hii tumetumia uanishaji wa sifa bainifu kwa mwelekeo wa Chomsky & Hale (1968).

Katika sura ya tatu tumelinganisha miundo ya silabi katika lugha ya Kikamba na lugha ya Kiswahili sanifu ikiwa kuzitofautisha na kuangazia mifano mbalimbali.

Katika sura ya nne tumechangana data. Katika kufanya hivyo tumezingatia mihimili minne ya nadharia ya lugha - kati kama ilivyopendekezwa na Selinker (1972)

Katika sura ya tano tumetoa muhtasari wa kazi nzima, hitimisho na mapendekezo. Hapa ndipo tumebaini ni kwa kiwango kipi tulivyoafikia malengo yetu.

SURA YA KWANZA

1.1 Utangulizi

Lugha ya Kiswahili ni muhimu sana na ina mawanda mapana sana kimatumizi. Lugha ya Kiswahili ina lahaja tofauti kama vile Kimvita, Kimtangata, Kiunguja na nyingine. Hata hivyo, utafiti wetu unalenga Kiswahili Sanifu ambacho kilisanifishwa kutokana na lahaja ya kiunguja.

Pamoja na kuwa Kiswahili ni lugha ya taifa, pia ni mojawapo ya lugha rasmi nchini Kenya Kiingereza kikiwa ya pili. Kiswahili ni lugha iliyoenea katika matumizi na ndio sababu hata sasa kinafanyiwa utafiti kwa sababu ya changamoto ambazo zimeikumba lugha hii. Ni lugha ambayo ni Lingua Franka kulingana na Habwe (1999). Ni lugha inayotumiwa katika shughuli za biashara na mawasiliano katika Afrika Mashariki.

Lugha ya Kiswahili katika nchi ya Tanzania hutumika kama lugha ya taifa na pia lugha rasmi. Kwa mujibu wa Massamba (1999) zaidi ya watu milioni sitini ulimwenguni hutumia lugha ya Kiswahili. Tukirejelea upande wa elimu; Kiswahili nchini Kenya kimekuzwa kwa mapana; Kwanza ni somo la lazima katika shule za msingi na za upili katika mfumo wa elimu unaotumika sasa wa 8-4-4. Aidha Kiswahili hufunzwa katika vyuo vya waalimu na pia vyuo vikuu. Katika mitihani ya kitaifa, somo la Kiswahili hutahiniwa katika darasa la nane na kidato cha nne hasa katika ufahamu, matumizi ya lugha na uandishi wa insha.

Hata hivyo kwa sasa, somo la lugha ya Kiswahili halijakuwa na matokeo ya kuridhisha kutoka mwaka wa 2006-2010 ikilinganishwa na somo la Kiingereza, aidha huenda ikawa matokeo hayo duni ni mojawapo ya vigezo vilivyochangia mwelekeo uliokuwa umechukuliwa na Baraza la mtihani la kitaifa wa kulifanya somo la Kiswahili kuwa la hiari katika mtihani wa darasa la nane, Kiswahili kikiwa kimepewa hadhi sawa na somo la lugha ishara. Huu ni mwelekeo uliopingwa sana na wataalamu wa lugha ya Kiswahili na ndiposa haukufua dafu. Hivyo matatizo ambayo yanaweza kuchangia kudunishwa kwa lugha hii yanapaswa kushughulikiwa ipasavyo kwa kuwa kama tulivyotaja ni lugha iliyo na hadhi na majukumu mengi nchini Kenya.

Kutokana na maelezo haya; ufunzaji wa lugha ya Kiswahili unapaswa kulenga hasa makosa yanayojitokeza katika maandishi ya wanafunzi wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili. Ni muhimu kubainisha makosa yenye hasa ya kifonolojia ambayo tutayashughulikia katika kazi za wanafunzi. Muhimu ni kuweza kuyabainisha wazi ili walimu wapate kuyaolewa na kuimarisha lugha. Matatizo haya hujitokeza katika muundo wa silabi.

1.2. Tatizo la Utafiti.

Kutokana na kazi za wanafunzi katika mitihani ya kitaifa, imedhihirika wazi kuwa makosa mbalimbali hujitokeza, hali ambayo inachangia matokeo duni kwenya mitihani ya Kiswahili. Baadhi ya makosa haya ni katika viwango vya Mofolojia,

Fonolojia, Sintaksia na tahajia. Kwa upande wa wazungumzaji ambao lugha yao ya kwanza ni Kikamba, makosa yaliyodhihirika zaidi ni ya Kifonolojia, ambapo miundo ya sauti inayotumika ni tofauti na iliyo katika Kiswahili Sanifu. Makosa haya yameibua hisia ya kuyashughulikia ili tuyabainishe wazi kuonyesha yanatokana na nini. Katika tafiti zilizofanywa makosa katika viwango vingine yameshughulikiwa lakini hapana utafiti wowote ulioshughulikia makosa ya Kifonolojia hasa katika kazi za wanafunzi ambao lugha yao ya kwanza ni Kikamba na wanajifunza Kiswahili kama lugha ya pili.

Hata hivyo tafiti zilizofanywa zimeegemea zaidi katika lugha ya Kiingereza kuliko za Kiswahili. Kwa mfano, Ndungu (1999) alichunguza makosa ya kisintaksia yanayofanywa na wanafunzi wanaojifunza Kiingereza kama lugha ya pili na lugha yao ya kwanza ni Kikuyu.

Tukirejelea upande wa Kiswahili, tafiti ambazo zimewahi kufanya kuhusu makosa yanayofanywa na wanafunzi wanaojifunza lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili, zimejikita zaidi katika matatizo ya kijumla, nyingine ni katika kiwango cha kimofolojia, kimofosintaksia, kwa mfano Rapando (2005) alichunguza makosa ya kimofo-sintaksia yanayofanywa na wanafunzi katika shule za upili jijini Nairobi. Mutugu (2001) alichunguza na kuainisha makosa ya kileksia yanayojitokeza katika insha za wanafunzi wa kidato cha pili.

Tukiangalia tafiti hizi, hapana utafiti wowote uliorejelea makosa ya kifonolojia yanayofanywa na wanafunzi wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili hasa lugha yao ya kwanza ikiwa ni Kikamba. Utafiti mmoja tu unaokaribiana na wetu na ambao utakuwa mchango mkubwa kwa kazi yetu, ni wa Musau (1993) ambaye alichunguza makosa ya kifonolojia lakini watafitiwa wanazungumza lugha ya kwanza tofauti tofauti; hali ambayo ni tofauti na utafiti wetu kwa kuwa tunarejelea wazungumzaji wa lugha ya Kikamba. Hivyo tatizo letu linahusu makosa ya kifonolojia yanvyojitokeza katika muundo wa silabi katika insha za wanafunzi walio katika viwango mbalimbali vya usomi.

Kutokana na tafiti zilizofanywa; matatizo yanayotokana na athari ya lugha ya kwanza uhitilafiana kutoka lugha moja hadi nyingine.

1.3. Madhumuni ya utafiti

- i. Kuchanganua makosa ya kifonolojia yanvyojitokeza katika - lugha kati ambayo ni lugha inayojitokeza badala ya lugha lengwa yaani Kiswahili sanifu.
- ii. Kubainisha sababu zinazochangia kuwepo na lugha - kati badala ya lugha lengwa.
- iii. Kuchunguza namna ambavyo lugha - kati imekiuka kanuni za kifonolojia za lugha ya Kiswahili sanifu.

1.4. Nadharia - Tete

- i. Mwanafunzi ambaye lugha yake ya kwanza ni Kikamba na anajifunza Kiswahili kama lugha ya pili, huishia kuzungumza au kuandika lugha kati ambayo siyo lugha ya Kiswahili sanifu iliyotarajiwa.
- ii. Lugha - kati hujitokeza badala ya Kswahili ambayo ni lugha lengwa kutokana na sababu mbalimbali.
- iii. Kanuni za Kifonolojia za Kiswahili Sanifu hukiukwa katika lugha – kati.

1.5. Sababu za Kushughulikia Tatizo

Uchunguzi wowote wa lugha ya Kiswahili ni muhimu kwa kuwa Kiswahili ni lugha inayotumiwa kwa mapana zaidi katika mawasiliano. Kwa mfano, wazungumzaji ambao lugha yao ya kwanza ni tofauti huweza kuwasiliana kwa lugha ya Kiswahili.

Hamazisho kubwa katika utafiti huu ni kwamba, Kiswahili ni mojawapo wa masomo ambayo hutahiniwa katika mitihani ya kitaifa. Zaidi ya hayo, Kiswahili ni lugha ambayo imepata changamoto nyingi sana kama tulivoyelezea awali. Ili tuweze kuhifadhi nafasi ya lugha ya Kiswahili, pana haja ya kubainisha na kuchanganua makosa yoyote yale yanayoweza kuchangi udunishaji wa lugha hii. Kazi za wanafunzi hasa katika insha zimedhihirisha makosa mengi ya kifonolojia, mengi yakiwa ni ya athari ya lugha ya kwanza. Hivyo utafiti huu utakuza uelewaji mwafaka wa sarufi ya lugha ya Kiswahili. Utafiti huu utajikita katika kiwango

cha fonolojia ili kuziba pengo la kuwa ni kiwango ambacho hakijafanyiwa utafiti wa kina. Utafiti huu utajikita katika nadharia ya lugha - kati, lugha ambayo hujitokeza badala ya lugha lengwa ambayo ni Kiswahili sanifu.

1.6. Upeo na Mipaka ya Utafiti

Katika utafiti huu, tutashughulikia makosa ya kifonolojia yanayofanywa na wazungumzaji wa lugha ya Kikamba kama lugha yao ya kwanza katika harakati ya kujifunza Kiswahili sanifu kama lugha yao ya pili. Tutajikita katika muundo wa silabi. Katika kufanya hivyo tutatumia insha za wanafunzi thelathini katika viwango vya darasa la sita, nane na kidato cha pili. Katika wilaya ya Makueni eneo la Mukuyuni. Hii ni kutokana na sababu kwamba kwa mujibu wa Selinker (1972) lugha – kati hubadilika badilika kutoka kiwango kimoja hadi kingine. Sehemu hii ya Makueni ni eneo ambalo wakazi wake hawana ukaribu wowote na wazungumzaji wa Kiswahili kama lugha ya kwanza. Nadharia tutakayoitumia ni nadharia ya lugha - kati iliyoasiwa na Selinker (1972), tutatumia mifanyiko mitano ya kisaikolojia iliyobainishwa katika nadharia hii.

1.7. Yaliyoandikwa Kuhusu Tatizo hili

Msingi wa utafiti juu ya namna wanafunzi hujifunza L2 katika nyanja za fonolojia, sintaksia, msamiati, uliwekwa na watafiti kama vile Selinker (1972), Corder (1967, 1981) na Krzeszowski (1974). Watafiti hawa walibainisha vipengele tofauti tofauti vya ujifunzaji wa L2. Maelezo katika utafiti wao

yamesaidia watafiti, waalimu katika kuendeleza hali ya ufunzaji na ujifunzaji wa lugha ya pili. Kuna mambo yaliyoandikwa kuhusu dhana ya lugha kati ikihusishwa na ujifunzaji wa L2, msingi wa lugha - kati na njia za uchanganuzi wa matatizo yanayojitokeza katika lugha - kati.

Yaliyoandikwa kuhusu uchanganuzi

Kulingana na tafiti zilizofanywa hapo mbeleni, uchanganuzi linganuzi ndio njia mwafaka ya kuchunguza matatizo yanayojitokeza kwa wanafunzi wanaojifunza L2. Tafiti ambazo zimefanywa kwa kutumia njia hii zimesaidia pakubwa katika kulinganisha miundo ya lugha tofauti kama vile Bowen na Martin (1965) Fisiak (1971).

Wanaouna mkono njia hii ya utafiti wanadai ya kwamba kwa kutumia uchanganuzi linganuzi miundo ya lugha mbili tofauti huweza kulinganishwa na mwishowe kuweza kugundua sehemu ambazo zinaweza kuwa na matatizo. Kwa mfano, kwa kutumia nadharia tete ya uchanganuzi linganuzi kwa kuelezea umuhimu au manufaa yake, Wardhaugh (1970) alieleza kwamba njia hii huweza kutumika kuwili. Udhaifu na uwezo wake. Njia hii ina uwezo wa kuonyesha ugumu unaopatikana katika ujifunzaji lugha kwa kuchunguza sifa za kimuundo za lugha zote mbili, hata kabla ya ujifunzaji wenyewe. Wazo hili limepingwa sana na wataalamu kama vile Ellis (1985) na Corder (1967).

Udhaifu wa njia hii unadhihirika katika maelezo yanayotolewa baada ya matatizo wenyewe kuonekana. Njia hii ilipingwa sana kwa kukosa mantiki hivyo watafiti wakaamua kutumia njia iliyotumiwa na watafiti waliochunguza ujifunzaji wa L1.

Uchanganuzi matatizo

Katika uchanganuzi huu watafiti walitaka kulinganisha njia zinazotumika katika kujifunza lugha ya kwanza na kujifunza lugha ya pili. Kulingana na maelezo yao, mikakati ambayo hutumiwa katika kujifunza L1, ndio hutumiwa katika L2. Isitoshe waligundua ya kwamba mikakati hii yote hutegemea umri, muktadha wa kujifunza L2 na historia ya L1 ya anayejifunza L2. Hali hii imeungwa mkono na Chomsky (1965).

Kulingana na maelezo ya Corder (1967) matatizo yanayojitokeza wakati mtu anajifunza L1 na L2 ni jambo la kawaida kuwepo kabla ya kuzoea matumizi kamili ya kanuni zinazoitawala lugha fulani. Corder anabainisha tofauti kati ya ‘makosa’ na ‘matatizo’. Anadai ya kwamba makosa ni matatizo yanayotokana na ule utendaji na hayana mpangilio wowote na yanaweza kutokea kwa hali zozote. Aidha kulingana na Corder, makosa hayana athari kubwa katika harakati za kujifunza lugha. Kwake Corder matatizo yanadhihirika kwa kuangalia umilisi wenyewe wa lugha na huwa na mpangilio.

Hivyo katika utafiti wetu tutarejelea zaidi dhana ya matatizo badala ya dhana ya makosa. Hii ni kutokana na maelezo ya dhana ya lugha - kati ambayo tumeeleza kuwa ni mfumo wa lugha ambao huwa na utaratibu fulani na uweza kuchunguzwa peke yake. Corder (1967; 167) anaeleza kuwa matatizo ya anayejifunza lugha ni muhimu kwa sababu humwezesha mtafiti kujua namna ambavyo watu hujifunza lugha. Isitoshe mtafiti anaweza kuelewa kiwango kile mwanafunzi alicho anayejifunza L2. Selinker (1972) anaeleza kwamba wanaisimu katika utafiti wao wanapaswa kuangalia harakati au mikakati ya kujifunza lugha kwa wanaojifunza L2.

Aidha mengi yameandikwa kuhusu namna ambavyo matatizo haya ya kifonolojia yanaweza kuelezw na pia kuyafafanua. Kwa mfano kuhusu njia za uchanganuzi Norrish (1983) katika Maina (1991; 20) anaelezea mielekeo miwili inayotumiwa katika uchanganuzi. Kwanza, anayechunguza matatizo haya hujitokeza na kategoria zake za matatizo. Pili, matatizo haya hupangwa katika makundi tofauti. Hivyo matatizo yenye ndio hutumiwa katika kuainisha kategoria yake. Katika utafiti wetu tutajifunga katika mwelekeo wa pili ambapo ni matatizo yenye we yatakayodhihirika kisha yatuelekeza katika kategoria fulani.

Kwa jumla, tafiti nyingi zimefanywa kuhusu suala la kujifunza L2. Musau (1993) alitafiti juu ya makosa ya kifonolojia ambayo hufanywa na wanafunzi wa Kiswahili. Utafiti huu ulihusu hasa wanafunzi ambao lugha yao ya kwanza ni

tofauti. Aidha, Musau alitumia wanafunzi wanaosomea taaluma ya ualimu wa shule za msingi nchini Kenya. Katika utafiti huu aligunduwa kwamba wanafunzi walio na L1 tofauti hutumia mikakati tofauti tofauti wanapojojifunza fonolojia ya Kiswahili kama L2. Kama tutakavyoona, utafiti huu ni tofauti sana na utafiti tutakaofanya. Kwanza, utafiti wetu haujifungi kwa wanafunzi ambao L1 ni tofauti bali tutajifunga kwa wanafunzi ambao lugha yao ya kwanza ni moja tu ambayo ni lugha ya Kikamba. Aidha, tutatafiti kwa kutumia wanafunzi katika shule za msingi na pia za upili tofauti na Musau (1993) aliyetumia wanafunzi wa vyuvo vyamafunzo ya ualimu.

Were (1994) alitafiti athari zinazotokana na L1 zinazodhihirika katika uandishi wa insha ya Kiswahili. Yeye alishughulikia makosa ya kimsamiati, tahajia na pia sarufi. Katika utafiti huu, Were alitambua kwamba kuna ile hali ya wanafunzi kujumlisha sheria na pia kuamisha kutoka L1 hadi L2 ambayo ni Kiswahili Sanifu. Hali hii ni tofauti na itakapodhihirika katika utafiti wetu. Kwanza utafiti wetu utajikita katika makosa ya kifonolojia wala sio kimofolojia na kama tutakavyoona tofauti na Were, makosa haya ya kifonolojia yanatokana na mambo kadha wala sio tu L1. Yeye aliangalia kipengele kimoja tu cha L1 kati ya vipengele vingine ambavyo huweza kuchangia katika matatizo ya kujifunza lugha ya pili.

 Rapando (2005) alitafiti makosa ya kimofo-sintaksia yanayojitokeza katika kazi za Kiswahili zilizoandikwa na wanafunzi wa shule za upili jijini Nairobi. Katika utafiti huu, Rapando aligundua kwamba baadhi ya makosa yanababishwa na L1 Kiingereza na Sheng. Aidha, ujumlishaji mno ulidhihirika kusababisha makosa hayo ya kimofo-sintaksia. Utafiti huu ni tofauti kabisa na tutakaofanya. Hii ni kwa kuwa katika utafiti wetu tutachunguza makosa ya kifonolojia yanayojitokeza kwa lugha kati ambayo hudhihirika kwa wanafunzi wanaojifunza Kiswahili kama L2. Hata hivyo kazi hii ya Rapando ina mchango mkubwa kwa utafiti wetu.

 Rapando (2005) katika ukusanyaji data, alitumia wanafunzi wa shule za upili za jijini Nairobi, tofauti na itakavyokuwa katika utafiti tutakaofanya. Pia wanafunzi tutakaotumia wanazungumza lugha ya kwanza iliyo sawa tofauti na wa jijini Nairobi. Zaidi ya hayo tutashirikisha wanafunzi katika shule za msingi. Usawa uliopo kwa kazi yetu ni kwamba tutachunguza kazi zilizoandikwa kama alivyofanya Rapando.

Kutokana na tafiti hizo zilizofanywa; inadhihirika wazi kwamba pana pengo ambalo linapaswa kuzibwa na ndio maana tukajitokeza na tatizo hili. Swala la fonolojia huwa ni tatizo kubwa sana na linahitaji kushughulikiwa, hasa miundo ya sauti mbalimbali. Ni tatizo ambalo limechangia sana kuwepo na lugha kati ambayo inaibuka kutokana na ile harakati ya kujifunza Kiswahili kama L2. Hivyo ili kuweza kuepuka tatizo hili, ni muhimu libainishwe wazi ndiposa iweze


kujulikana namna ambavyo wanafunzi na pia walimu wanaweza kukabiliana na matatizo haya, hasa tukirejelea wanafunzi ambao lugha yao ya kwanza ni kikamba na wanajifunza Kiswahili sanifu kama L2.

1.8. Msingi wa Nadharia

Ili kuimarisha kujifunza kwa lugha ya pili katika mazingira ya darasani, utafiti kuhusu lugha - kati inayoandikwa na wanafunzi wanaojifunza L2 ni muhimu sana. Utafiti huu utatumia ile njia ya kuchanganua matatizo ya kifonolojia yanayojitokeza katika lugha kati. Hivyo, kutokana na hali hii utafiti wetu utajifunga katika nadharia ya lugha kati. Hii ni kwa kuwa matatizo tutakayochanganua yanadhihirika katika lugha hii.

Kwa mujibu wa Selinker (1962, 1972) lugha - kati ni lugha inayoundwa na wanaojifunza L2 katika harakati zao za kutaka kufikia lugha lengwa. Anaendelea na kusema kuwa, lugha - kati ni mfumo tofauti wa kiisimu ambao unaibuka kutokana na ile harakati ya kujifunza L2. Kulingana na Selinker (1972), mfumo huu tofauti wa kiisimu unaweza kuchunguzwa kwa kushirikisha wanaojifunza L2 katika maandishi au mazungumzo. Anasema kuwa, lugha kati hubadilikabadilika kulingana na muktadha; jambo ambalo limeungwa mkono na Tarone (1979). Lugha - kati hubadilika pia kutoka kiwango kimoja hadi kingine mpaka mwanafunzi anafikia ule umilisi unaotarajiwa wa L2. Ni lugha inayohusu mzungumzaji mmoja yaani anayejifunza L2. Mabadiliko haya ya lugha kati huwa

ni ya kiisimu, kisaikolojia na katika muktadha wa jamii. Mabadiliko ya kiisimu huwa ni yale ya matamshi ya fonimu ambayo si rahisi kutamkwa kutegemea na mahali fonimu hiyo inajitokeza, aidha mwanzo au mwishoni mwa silabi. Katika maelezo ya lugha - kati, mchoro ufuatao ulitumika.



Maelezo mengine ya lugha - kati yalitolewa na Corder (1967), Corder anasema kwamba katika lugha ya mwanafunzi anayejifunza lugha fulani, kuna muundo fulani ambao hujitokeza na pia mikakati fulani ya kujifunza ile lugha. ~~matatizo~~ ambayo yana~~adh~~hirika katika muundo huu wa lugha ndio dhihirisho ya kwamba mwanafunzi yu katika harakati za kujifunza L2. Kutokana na maelezo haya, uchanganuzi wa matatizo haya ukawa ndio unatumika sana na walimu darasani na vilevile watafiti.

Aidha, Dulay na Burt (1974) wanaeleza kwamba, uchunguzi wa lugha uliofanywa ulidhihirisha kwamba matatizo ya lugha katika mazungumzo yalikuwa tofauti na matatizo ya lugha katika maandishi. Hata hivyo, kulingana na maandishi mengi, dhana ya lugha- kati ilitokana na Selinker (1969). Watafiti wengi waliotafiti ujifunzaji wa L2 wametumia sana dhana ya lugha - kati.

Selinker (1972) alibainisha mifanyiko mitano ya kisaikolojia ambayo ni muhimu katika uchanganuzi wowote wa lugha - kati. Mifanyiko hii ni kama ifuatayo;

1. Uhamishaji lugha ambapo kanuni na mifumo ya lugha - kati yaweza kutokana na L1.
2. Uhamishaji wa ufundishaji hii ni kutokana na ile hali ya wanaofundisha L2 kukosa ule umilisi wa lugha yenyewe; kutumia mbinu finyu za ufundishaji na kukosa vifaa mwafaka nya kufunzia.
3. Mikakati ya kujifunza L2. Baadhi ya elementi zinazopatikana katika lugha - kati hutokana na mwelekeo mahususi dhidi ya yale wanafunzi watajifunza.
4. Mikakati ya mawasiliano katika L2. Elementi za lugha - kati hutokana na njia mahususi ambazo watu hujifunza ili kuweza kuwasiliana na wazungumzaji asilia wa lugha lengwa.
5. Ujumlishaji mno- kanuni za lugha lengwa hujumlishwa hivyo hutumika kiholelaholela yaani pasipofaa.

Kulingana na mifanyiko hii, inadhihirika wazi kwamba lugha - kati inaweza kuangaliwa kivyake kama kiwango kimoja cha umilisi wa L2. Pia inadhihirika kwamba mfumo unaojitekeza katika lugha - kati sio kamili kama ulivyo katika L2. Aidha, muundo wake huenda ukaathiriwa na L1, hii ni kutokana na ile hali ya mwanafunzi kutumia kanuni za L1 ambazo amezizoea na hivyo kuvunja kanuni za lugha lengwa.

Katika utafiti wetu, hatutakuwa tunalinganisha lugha mbili ili kutambua matatizo ya kiisimu na ndiposa mtazamo wa uchanganuzi linganishi haufungani na utafiti wetu. Aidha, utendaji wa wanafunzi utakaodhihirika darasani hauwezi kuchunguzwa kwa kutumia uchanganuzi linganuzi.

Katika utafiti wetu tutatumia mtazamo wa uchanganuzi wa makosa kwa kuwa ndio mwelekeo ambao hutilia maanani matatizo yote yanayosababishwa na mambo mengine mbali na athari za L1. Uchanganuzi wa matatizo pia uwezekana zaidi katika lugha kati ambapo matatizo yenye hudhihirika.

Aidha, kulingana na maelezo ya nadharia ya lugha - kati, mifanyiko tuliyotaja mitano inaweza kuchuguzwa kwa kurejelea lugha - kati. Ni katika lugha - kati ambapo uhamishaji wa lugha, ufundishaji utadhihirika. Pia mikakati ya ufunzaji na ~~h~~ujifunzaji itadhihirika wazi katika lugha - kati. Kwa jumla mifanyiko hii inachangia pakubwa katika makosa ya kifonolojia ambayo ndio kiini cha utafiti wetu.

1.9. Njia za utafiti

a) Ukusanyaji data

Nyanjani tutatumia Insha kumi za wanafunzi wa darasa la sita, saba na kidato cha tatu. Kwa jumla tutatumia Insha thelathini. Katiki utafiti huu tutatumia sampuli

lengwa ambapo Insha za wanafunzi wa kwanza wawili, watano wa saba, kumi na watano, wa ishirini, wa ishirini na tano na wawili wa thelathini na mbili.

b) Uchanganuzi data

Tutasahihisha insha hizo kwa kutia makini kwenye makosa yanayojitokeza ya kifonolojia. Tutafanya hivyo kwa kuzingatia vipengele vya nadharia ya lugha - kati hasa katika mifanyiko ile mitano ya kisaikolojia ambayo ni muhimu katika uchangazi wa lugha kati.

SURA YA PILI

FONIMU ZA KISWAHILI SANIFU NA KIKAMBA

2.1. Utangulizi

Ni muhimu kutoa ufanuzi wa uwanja unaohusu vipengele hivi, yaani fonolojia. Fonolojia ni tawi la isimu linaloshughulikia uchambuzi wa mfumo wa sauti zinazotumiwa katika lugha fulani Tuki (1999; 46).

Kiswahili na Kikamba ni lugha asilia za Kibantu, zinaweza kuwa na sauti zinazowiana, kwa sababu lugha za binadamu hutumia sauti zilizochotwa kutoka kwenye ghala moja, hivyo tunaweza kutajia kwamba zina sifa za sauti za kimsingi zinazowiana. Hata hivyo, lugha mbili asilia haziwezi kuwa sawa katika vipengele vyote vya sauti.

Kwa sababu kipengele cha uchunguzi katika fonolojia ni fonimu, ni muhimu kutoa kijelezi chake. Fonimu ni kipashio kidogo babisa cha kifonolojia kinachobadili maana ya neon Tuki (1999; 45). Fonimu pia ni kitamkwa kilicho bainifu katika lugha fulani maalum Massamba et al (2004). Kwa mfano, fonimu /p/ /b/ katika Kiswahili sanifu ni sauti bainifu. Panda na banda - /p/ na /b/

Ili kuweza kuieleza lugha vizuri ni muhimu kuanzia kwenye kiwango cha sauti za hiyo lugha. Wataalamu wengi wanazungumzia juu ya sauti za lugha za

Kiswahili sanifu kwa kiwango kikubwa, hawa ni kama vile Habwe na Karanja (2004), Kihore et al (2001). Massamba et al 2004, Iribemwangi (2008) miongoni mwa wengine. Kwa misingi hiyo imetubidi kuzungumzia fonimu za Kiswahili sanifu katika sehemu ifuatayo.

2.2 Sifa bainifu za Fonimu za Kiswahili

Fonimu za Kiswahili zitatusaidia kwa sababu madhumuni ya sura hii ni kuainisha sauti za lugha za Kiswahili sanifu na Kikamba. Tutaangalia vipengele vyatimsingi vyatimfonolojia ambavyo kulingana na Iribemwangi (2008) ni vyatimaina tatu;

- i. Konsonanti
- ii. Irabu
- iii. Nusu irabu

Aidha katika sura hii tutaangalia sifa bainifu katika fonimu hizi. Muundo wa silabi pia utakuwa ni muhimu ambapo tutakuja kuona namna sauti uunda silabi katika lugha ya Kiswahili sanifu na Kikamba.

2.2.1 Fonimu za Konsonanti

Kwa kurejelea idadi ya konsonanti za Kiswahili sanifu, wataalamu wengi wana maoni tofauti. Iribemwangi (2008), ameainisha konsonanti 25, Massamba na wenzake (2004), wameainisha 23. Polome (1967) naye ameainisha 24. Katika utafiti huu tunachukua mwelekeo wa uainishaji wa Iribemwangi (2008).

Ifahamike kwamba idadi yake ni ishirini na tano. Hii ni kwa kuwa kulingana na utafiti huu, uainishaji huu utatufaa sana.

Uainishaji huu ni kama ufuatao:

Vipasuo

| | |
|---|---|
| $\begin{bmatrix} /p/ \\ +kons \\ +kip \\ +midomo \\ -ghuna \end{bmatrix}$ | $\begin{bmatrix} /b/ \\ +kons \\ +kip \\ +midomo \\ +ghuna \end{bmatrix}$ |
|---|---|

| | |
|---|---|
| $\begin{bmatrix} /t/ \\ +kons \\ +kip \\ +midomo \\ -ghuna \end{bmatrix}$ | $\begin{bmatrix} /d/ \\ +kons \\ +kip \\ +midomo \\ +ghuna \end{bmatrix}$ |
|---|---|

| | |
|--|--|
| $\begin{bmatrix} /k/ \\ +kons \\ +kip \\ +kaakaa\ laini \\ -ghuna \end{bmatrix}$ | $\begin{bmatrix} /g/ \\ +kons \\ +kip \\ +kaakaa\ laini \\ +ghuna \end{bmatrix}$ |
|--|--|

Sauti hizi pia huitwa vizuiwa. Huwa ni vipasuo kwa sababu wakati wa kuzitamka hewa huzuiwa katika ala za matamshi kisha huachiliwa kwa ghafla hivi kwamba sauti hutoka kwa mpasuo.

Vizuiwa kwamizwa

Katika lugha ya Kiswahili, hizi ni sauti ambazo wakati wa kuzitamka mkondo hewa huzuiwa kisha kuachiliwa taratibu na kutoka kwa mkwamzo.

| |
|-----------------------------|
| /tʃ/ |
| + <i>kons</i> |
| + <i>kizuiwa - kwamizwa</i> |
| + <i>kaakaa gumu</i> |
| - <i>ghuna</i> |

| |
|-----------------------------|
| /ʃ/ |
| + <i>kons</i> |
| + <i>kizuiwa - kwamizwa</i> |
| + <i>kaakaa gumu</i> |
| + <i>ghuna</i> |

Vikwamizwa

Katika Kiswahili sanifu hizi ni sauti ambazo wakati wa kutamkwa ala za matamshi hukaribiana sana hivi kwamba hewa hupitishwa katikati ya ala hizo hivi sauti hutokea kwa kikwamizo.

| |
|---------------------|
| /s/ |
| + <i>kons</i> |
| + <i>kikwamizwa</i> |
| + <i>ufizi</i> |
| - <i>ghuna</i> |

| |
|---------------------|
| /z/ |
| + <i>kons</i> |
| + <i>kikwamizwa</i> |
| + <i>ufizi</i> |
| + <i>ghuna</i> |

| |
|------------------------|
| /f/ |
| + <i>kons</i> |
| + <i>kikwamizwa</i> |
| + <i>midomo - meno</i> |
| - <i>ghuna</i> |

| |
|------------------------|
| /v/ |
| + <i>kons</i> |
| + <i>kikwamizwa</i> |
| + <i>midomo - meno</i> |
| + <i>ghuna</i> |

| |
|--|
| $/θ/$ + <i>kons</i> + <i>kikwamizwa</i> + <i>meno</i> - <i>ghuna</i> |
|--|

| |
|--|
| $/ð/$ + <i>kons</i> + <i>kikwamizwa</i> + <i>meno</i> + <i>ghuna</i> |
|--|

| |
|---|
| $/ʃ/$ + <i>kons</i> + <i>kikwamizwa</i> + <i>kaakaa gumu</i> - <i>ghuna</i> |
|---|

| |
|--|
| $/X/$ + <i>kons</i> + <i>kikwamizwa</i> + <i>kaakaa laini</i> - <i>ghuna</i> |
|--|

| |
|--|
| $/χ/$ + <i>kons</i> + <i>kikwamizwa</i> + <i>kaakaa laini</i> + <i>ghuna</i> |
|--|

| |
|--|
| $/h/$ + <i>kons</i> + <i>kizuiwakwamizwa</i> + <i>glota</i> + <i>ghuna</i> |
|--|

Nazali

Hizi ni fonimu za Kiswahili ambapo wakati wa kuzitamka hewa nyingi hupitia chemba cha pua hivi kwamba sauti hizi huwa na king'ong'o.

| |
|-----------------|
| $/m/$ |
| + <i>kons</i> |
| + <i>nazali</i> |
| + <i>midomo</i> |
| + <i>ghuna</i> |

| |
|-----------------|
| $/n/$ |
| + <i>kons</i> |
| + <i>nazali</i> |
| + <i>ufizi</i> |
| + <i>ghuna</i> |

| |
|----------------------|
| $/ʃ/$ |
| + <i>kons</i> |
| + <i>nazali</i> |
| + <i>midomo meno</i> |
| + <i>ghuna</i> |

| |
|-----------------------|
| $/ʒ/$ |
| + <i>kons</i> |
| + <i>nazali</i> |
| + <i>kaakaa laini</i> |
| + <i>ghuna</i> |

h

| |
|-----------------------|
| $/h/$ |
| + <i>kons</i> |
| + <i>nazali</i> |
| + <i>kaakaa laini</i> |
| + <i>ghuna</i> |

Japo bado kuna utata kuhusu fonimu /M/ ni fonimu ambayo inatumika katika Kiswahili sanifu. Iribemwangi (2008:54) anasema kwamba ni fonimu ambayo haipatikani katika jazi mlinganuofinyu hivyo kuna utata kama ni fonimu au ni alofoni ya fonimu /m/. Hata hivyo ni muhimu kufahamisha kwamba ni sauti inayotumika katika Kiswahili sanifu.

Vitambaza

Hizi ni sauti ambazo wakati wa kuzitamka hewa hupitishwa kando kando ya ala za matamshi. Kiswahili sanifu kina kitambaza kimoja.

| | |
|--------------------|--|
| /l/ | |
| + <i>kons</i> | |
| + <i>kitambaza</i> | |
| + <i>ufizi</i> | |
| + <i>ghuna</i> | |

Vimadende

Wakati wa kuzitamka sauti hizi, ulimi hupigapiga kwenye ufizi .Kiswahili sanifu kina kimadende kimoja /r/.

| | |
|--------------------|--|
| /r/ | |
| + <i>kons</i> | |
| + <i>kimadende</i> | |
| + <i>ufizi</i> | |
| + <i>ghuna</i> | |

Viyeyusho /nusu irabu

Hizi ni sauti ambazo wakati wa kutamka hewa haizuiliwi kama katika kutamka konsonanti na pia hewa haiwachiliwi kama katika irabu. Kiswahili sanifu kina nusu irabu mbili /w/.¹⁴/

$$\left[\begin{array}{l} /w/ \\ +nusu\ irabu \\ +midomo \\ +ghuna \end{array} \right]$$

$$\left[\begin{array}{l} /j/ \\ +nusu\ irabu \\ +\underline{midomo} \\ +ghuna \end{array} \right]$$

Jedwali 1:


Jedwali la Konsonanti za Kiswahili Sanifu.

| Mahali pa kutamkwa | Jinsi ya kutamkwa | | | | | | |
|--------------------|-------------------|-------------------|-------------|---------|------------|------------|--|
| | Vipasu o | Vizuiwa-kwamiz wa | vikwamiz wa | naza li | kitamba za | kimadan de | |
| Midomo | /p/ / b/ | | | /m/ | | | |
| Midomome no | | | /f/ /v/ | /M/ | | | |
| Meno | | | /θ/ /ð/ | | | | |
| Kaakaa+ufi zi | | | /S/ | | | | |
| Ufizi | /t/ /d/ | | /s/ /z/ | /ʃ/ | /l/ | /r/ | |
| Kaakaagum u | | /ʃ/ /ʒ/ | | /j/ | | | |
| Kaakaalaini | /k/ /g/ | | /χ/ /ʒ/ | /n/ | | | |
| Glota | | | /h/ | | | | |
| Jumla | 6 | 2 | 10 | 5 | 1 | 1 | |

(25)

2.2.2 Fonimu za Irabu za Kiswahili Sanifu

Ili kuunda silabi konsonanti huungana na irabu, hivyo ni muhimu kuainisha irabu za Kiswahili sanifu. Tunafanya hivyo kwa sababu baadaye tutaunganisha irabu hizi na konsonanti kuunda silabi. Ni katika muungano huo ndipo tutabainisha matatizo ya kifonolojia yanavyojitokeza. Kulingana na (Mathews 1997:384), lugha nyingi za kibantu zina irabu saba ilhali kiswahili sanifu kina irabu tano. Irabu hizi huweza kuelezwu kwa kutumia mchoro ufuatao; kulingana na Polome (1967), IribiMwangi (2008), Mathews (1997) mionganoni mwa wengine.



| | |
|--|--|
| $\left[\begin{array}{l} /i/ \\ +irabu \\ +mbele \\ +juu \\ -mviringo \end{array} \right]$ | $\left[\begin{array}{l} /u/ \\ +irabu \\ +nyuma \\ +juu \\ +mviringo \end{array} \right]$ |
|--|--|

| | |
|---|---|
| $/ɛ/$ + <i>irabu</i> + <i>mbele</i> + <i>kati</i> - <i>mviringo</i> | $/ɔ/$ + <i>irabu</i> + <i>nyuma</i> + <i>kati</i> + <i>mviringo</i> |
|---|---|

| |
|---|
| $/a/$ + <i>irabu</i> + <i>kati</i> + <i>chini</i> - <i>mviringo</i> |
|---|

Jedwali 2:

Jedwali la irabu za Kiswahili Sanifu

| irabu | /i/ | /u/ | /ɛ/ | /ɔ/ | /a/ |
|-----------------|-----|-----|-----|-----|-----|
| Juu | + | + | - | - | - |
| Chini | - | - | - | - | + |
| Nyuma | - | + | - | + | - |
| Mbele | + | - | + | - | - |
| Mviringo | - | + | - | + | - |
| Kaze | + | + | - | - | + |

Ni muhimu kutaja kwamba lugha nyingi za Kibantu huwa na mfumo wa irabu saba. Hata hivyo japo Kiswahili ni lugha ya kibantu kina mfumo wa irabu tano.

Katika kuhitimisha sehemu hii ni bora kufahamisha kwamba tumetumia uainishaji wa fonimu wa Chomsky & Hale (1968) kama wanavyonukuliwa na Iribemwangi (2008:52). Uainishaji huu ni ule ambao umekita katika fonetiki matamshi ambao ndio unaopendelea sana na wanafonolojia.

Kulingana na uainishaji huu ni wazi kuwa kadri irabu inavyokuwa ya juu ndivyo inavyokuwa ya mbele. Hivyo irabu zote za mbele ni [-mviringo] na zile za nyuma ni [+mviringo]. Hata hivyo irabu ya juu huwa ni ya mviringo zaidi kuliko ya chini mathalani /u/ ni ya mviringo zaidi kuliko /ɔ/ hata ingawa irabu hizo zote ni [+nyuma]. Vilevile irabu za juu mbele huwa ni za mviringo zaidi kuliko za chini mbele.

2.3 Sifa Bainifu za Fonimu za Kikamba

Fonolojia kiarudhi ya Kikamba inaonekana imeshughulikiwa zaidi kuliko fonolojia vipandesauti. Hata hivyo Maundu (2001) ameshughulikia mabadiliko ya konsonanti za Kikamba. Sehemu hii itatoa mchango mkubwa katika kazi hii kwa sababu fonimu zitaainishwa kwa sifa bainifu na kufanya hivyo kutatuonesha sifa za fonimu ambazo ni za fonimu za kikamba zitakavyokuwa zinahamishwa na watumizi lugha ya Kiswahili ambao wanazungumza kikamba kama lugha yao ya kwanza.

2.3.1 Konsonanti

Kikamba kina vipande sauti ambavyo vinaweza kugawika katika makundi mawili, konsonanti na irabu. Mgao huu unatumika sana katika lugha nyingi kutegemea kiwango cha kutatizwa kwa mkondohewa wakati wa kuzitamka sauti hizi, mawazo haya yamewahi kutolewa pia na Abercrombie (1966), Chomsky na Hale (1968), Ladefoged (1982),(1971).

Uainishaji wa Konsonanti za Kikamba

Hapa tunashughulikia konsonanti zilizopo katika kikamba. Ni muhimu kutambua kwamba konsonanti kama vile /b/ /d/ /g/ /z/ na /dz/ hazitokei mwanzoni mwa neno bali hutanguliwa na vipandesauti vya nazali. Kimsingi, kikamba kina konsonanti kumi na nane, kulingana na Mutie (2001:6)

| |
|------------------|
| /t/ |
| + <i>kipasuo</i> |
| + <i>ufizi</i> |
| - <i>mghuno</i> |

| |
|-----------------------|
| /k/ |
| + <i>kipasuo</i> |
| + <i>kaakaa laini</i> |
| - <i>mghuno</i> |

| |
|-----------------|
| /m/ |
| + <i>nazali</i> |
| + <i>midomo</i> |
| + <i>mghuno</i> |

| |
|-----------------------|
| /ʃ/ |
| + <i>nazali</i> |
| + <i>kaakaa laini</i> |
| + <i>mghuno</i> |

| | |
|-----------------|-----------------------|
| $/n/$ | $/h/$ |
| + <i>nazali</i> | + <i>nazali</i> |
| + <i>ufizi</i> | + <i>kaakaa laini</i> |
| + <i>mghuno</i> | + <i>mghuno</i> |

| | |
|----------------------|---------------------|
| $/v/$ | $/θ/$ |
| + <i>kikwamizwa</i> | + <i>kikwamizwa</i> |
| + <i>midomo meno</i> | + <i>meno</i> |
| + <i>mghuno</i> | - <i>mghuno</i> |

| | |
|--------------------------------|-----------------------|
| $/l/$ | $/w/$ |
| + <i>kifulizwa / kitambaza</i> | + <i>kifulizwa</i> |
| + <i>ufizi</i> | + <i>midomo ufizi</i> |
| + <i>mghuno</i> | + <i>mghuno</i> |

| | |
|---------------------|--------------------------|
| $/s/$ | $/j/$ |
| + <i>kikwamizwa</i> | + <i>kifulizwa</i> |
| + <i>ufizi</i> | + <i>mbele ya kaakaa</i> |
| - <i>mghuno</i> | + <i>mghuno</i> |

| | |
|--------------------------|--|
| /t/ | |
| + <i>kikwamizwa</i> | |
| + <i>mbele ya kaakaa</i> | |
| + <i>mghuno</i> | |

| | |
|------------------|--|
| /b/ | |
| + <i>kipasuo</i> | |
| + <i>midomo</i> | |
| + <i>mghuno</i> | |

| | |
|------------------|--|
| /d/ | |
| + <i>kipasuo</i> | |
| + <i>ufizi</i> | |
| + <i>mghuno</i> | |

| | |
|----------------------|--|
| /g/ | |
| + <i>kipasuo</i> | |
| + <i>kaakaa gumu</i> | |
| + <i>mghuno</i> | |

| | |
|---------------------|--|
| /z/ | |
| + <i>kikwamizwa</i> | |
| + <i>ufizi</i> | |
| + <i>mghuno</i> | |

| | |
|-------------------------------|--|
| /dz/ | |
| + <i>kizuiwa kwamizwa</i> | |
| + <i>mbele ya kaakaa gumu</i> | |
| + <i>mghuno</i> | |

Jedwali 3:

Jedwali la Konsonanti za Kikamba

| | | | | | | |
|---------------------|-------------------|------------------|------------|--------------|-----------|-----------|
| Mahali pa kutamkwa | Jinsi ya kutamkwa | | | | | |
| | Vipasuo | Vizuiwa-kwamizwa | Vikwamizwa | Nazali | Kitambaza | Vifulizwa |
| Midomo | /b/ | | | /m/ | | /w/ |
| Midomomeno | | | /v/ | | | |
| Meno | | | /θ/ | | | |
| <u>Kaakaa+ufizi</u> | | | | | | |
| Ufizi | /t/ /d/ | | /s/ /z/ | /n/ | /l/ | |
| Kaakaagumu | /g/ | /dz/ | /tʃ/ | /ʃ/ <i>r</i> | | / j/ |
| Kaakaalaini | /k/ | | | /f/ | | |
| Jumla | 5 | 1 | 5 | 4 | 1 | 2 (18) |

Kama tulivyokwisha taja konsonanti /b/, /d/ /g/ /z/ na /dz/ hutokea baada ya kutanguliwa na nazali, hivyo nazali hizi ambazo zimetangulia konsonanti hupokezwa sifa za mahali pa kutamkiwa pa konsonanti hizi. Hivyo mfanyiko unaotokea ni ule wa usilimisho. Katika kikamba mfuatano wa konsonanti unaokubalika ni ule wa konsonanti mbili kufuatana na hutokea unazalishaji pamwe wa nazali; yaani /mb/, /nd/, /nz/ na / *=* /. Hali hii hujitokeza hivyo kwa sababu za kurahisisha matamshi.


Kuna viyeyusho viwili katika kikamba, navyo ni /w/ na /j/.

2.4 Uainishaji wa Irabu

Kikamba kina irabu Saba. Sifa za kubainisha irabu ni kama vile. Mwinuko wa ulimi, mkao wa mdomo, sehemu ya ulimi. Kwa kutumia sifa hizi kikamba kina irabu zifuatazo;

/a, ε, e, i, ɔ, o, u/

Katika uainishaji, tumetumia sifa bainifu za irabu ambazo ni; mwinuko wa ulimi, sehemu ya ulimi na mkao wa mdomo wakati wa kutamka.



| | |
|-------------------|-------------------|
| $/i/$ | $/e/$ |
| + <i>irabu</i> | + <i>irabu</i> |
| + <i>mbele</i> | + <i>mbele</i> |
| + <i>juu</i> | + <i>nusu juu</i> |
| - <i>mviringo</i> | - <i>mviringo</i> |

| | |
|-------------------|-------------------|
| $/ɛ/$ | $/u/$ |
| + <i>irabu</i> | + <i>irabu</i> |
| + <i>mbele</i> | + <i>nyuma</i> |
| - <i>chini</i> | + <i>juu</i> |
| - <i>mviringo</i> | + <i>mviringo</i> |

| | |
|-------------------|-------------------|
| $/ɔ/$ | $/ɔ/$ |
| + <i>irabu</i> | + <i>irabu</i> |
| + <i>nyuma</i> | + <i>nyuma</i> |
| - <i>nusu juu</i> | - <i>chini</i> |
| + <i>mviringo</i> | + <i>mviringo</i> |

| |
|-------------------|
| $/ɑ/$ |
| + <i>irabu</i> |
| + <i>chini</i> |
| - <i>mbele</i> |
| - <i>mviringo</i> |

Jedwali 4:

Jedwali la Irabu za Kikamba

| Irabu | /i/ | /e/ | /ɛ/ | /u/ | /o/ | /ɔ/ | /a/ |
|----------|-----|-----|-----|-----|-----|-----|-----|
| Juu | + | + | - | + | + | - | - |
| Chini | - | - | - | - | - | - | + |
| Nyuma | - | - | - | + | + | + | - |
| Mbele | + | + | + | - | - | - | - |
| Mviringo | - | - | - | + | + | + | - |
| Kaze | + | + | - | + | - | - | + |

Kulingana na Lindlon (1926) Kikamba kina aina zote za irabuunganifu.

Mifano ya irabuunganifu za kushuka;

Kikamba Kiswahili

- | | |
|---------|--------|
| 1. mwəi | mwezi |
| 2. təi | huruma |
| 3. mbui | mbuzi |

Kumbuka kwamba, kulingana na Lindlon (1926) irabu fupi inapotanguliwa na irabu nyingine Irabuunganifu huundwa.

Irabuunganifu za kupanda huyeyushwa, aidha uyeyushaji ni mfanyiko wa kimsingi katika lugha ya Kikamba.

Kwa mfano;

| <u>Kikamba</u> | <u>Kiswahili</u> |
|--------------------------|------------------|
| /ke\$ a \$ ma/ - [tʃama] | - muungano |
| /ke \$ɔg / - [tʃɔ:g] | - kichwa |

Vile vile kuna irabuunganifu tatu ambazo pia huyeyushwa.

Kwa mfano;

| <u>Kikamba</u> | <u>Kiswahili</u> |
|----------------------|------------------|
| /ke + a / - [t a:ɔ] | - daraja |
| /ke + a / - [ta:ɔ] | - nini |

Hitimisho

Katika sura hii tumeshughulikia fonimu za Kiswahili sanifu ambayo ndiyo lugha mwongozo na fonimu za kikamba . Tumebainisha sifa bainifu za fonimu za konsonanti na irabu za lugha hizi mbili. Ni kutokana na sifa hizi bainifu tutakaopata mwongozo wa muundo wa silabi pamoja na kubaini makosa yanayofanywa ya kifonolojia. Kulingana na nadharia tumizi ya lugha kati kutokana na mwongozo huu, ndipo baadhi ya mifanyiko ya kisaikolojia kulingana

na Selinker (1972) itajitokeza katika uchanganuzi wetu wa lugha kati. Hali hii itatusaidia kujua ni kwa kiasi gani lugha kati imekiuka kanuni za lugha lengwa ambayo ni Kiswahili sanifu. Sura hii pia imetupa mwangaza wa namna lugha hizi zinavyotofautiana na kuwiana katika vipengele vya kifonolojia japo lugha hizi mbili ni za kibantu.

SURA YA TATU

MUUNDO WA SILABI KATIKA LUGHA YA KISWAHILI SANIFU NA

KIKAMBA

3.0. Utangulizi

Katika sehemu hii tutajadili tofauti za kimuundo kati ya Kiswahili na Kikamba. Tofauti hizi zitajikita katika kiwango cha fonolojia. Hii ni kwa kuwa, tunajuwa matatizo mengi yanayowakumba wazungumzaji asilia wa lugha ya kikamba wanapojifunza lugha ya Kiswahili hutokana na tofauti za kimuundo zilizopo kati ya lugha hizi mbili; sura hii ni msingi wa yale tutakaojadili katika sura zitakazofuata.

Kuna aina mbili za silabi; silabi huru na silabi fungo. Silabi huru ni zile ambazo mara nyingi huishia na irabu. Hizi huwa na msikiko mkubwa zaidi. Silabi fungo ni zile ambazo huishia na konsonanti. Hata hivyo kulingana na maelezo ya wataalamu tofauti, kila silabi huwa na irabu kama kilele chake yaani irabu ni kitu muhimu sana katika silabi. Aidha kuna lugha ambazo hutumia baadhi ya konsonanti pekee kama silabi. Kwa mfano katika Kiswahili sanifu nazali /m/ na /n/ husimama peke yake kama silabi.

Msingi wa miundo ya silabi za Kiswahili sanifu ni miundo ya silabi za kibantu, Massamba et al (2004). Katika muundo wa silabi katika lugha ya Kiswahili, kuna miundo ya silabi iliyotokana na lugha za kigeni na inadhihirika katika maneno ya

mkopo. Vilevile pana miundo ya silabi asilia lugha ya Kiswahili. Hivyo lugha mbalimbali hutofautiana kwani kila moja ina mfumo wake na muundo wake wa silabi. Lugha ya Kiswahili sanifu ina miundo mbalimbali ya silabi.

3.1. Muundo wa Silabi katika lugha ya Kiswahili

Zipo kanuni zinazotawala mfuatano wa konsonanti na irabu katika kujenga maneno ya Kiswahili. Watumizi wa lugha hutamka sauti katika silabi. Kila lugha ina muundo wake wa silabi. Silabi hizi huundwa kwa kuleta pamoja fonimu katika mazingira fulani ili kuwepo na ruwaza ambayo inaweza kutamkika. Mabadiliko ya sauti hudhihirika wakati fonimu hizi zinaletwa pamoja. Katamba (1989) ni katika muundo wa silabi, ndio tunapata kanuni ambazo zinatawala matumizi ya lugha fulani katika harakati za kujaribu kuleta sauti fulani pamoja ili kuunda silabi. Muungano wa sauti zozote katika lugha fulani hutegemea muundo wa silabi katika lugha hiyo. Kulingana na Iribemwangi (2010) tuna miundo tisa ya silabi katika lugha ya Kiswahili.

i. Muundo wa Silabi pendwa ni ule wa konsonanti irabu K\$I

Huu ndio muundo wa silabi ambao hutumika sana katika lugha za kibantu. Aidha muundo huu wa silabi ndio wa kimsingi katika lugha ya Kiswahili sanifu. Kwa mfano maneno yafuatayo yameundwa kwa muundo huu.

Ta\$la\$ka

Ho\$tu\$ba

ii. Muundo wa Konsonanti Konsonanti irabu K\$K\$I

Katika muundo huu nafasi ya kwanza huchukuliwa na mojawapo wa nazali tano. Kisha inafuatwa na vikwamizwa au vipasuo, nafasi ya mwisho huweza kuchukuliwa na mojawapo ya irabu tano.

Kwa mfano;

m\$vu\$vi

n\$dε\$gε

iii. Muundo wa Konsonanti nusu irabu irabu irabu K\$%I\$I

Yaani konsonanti tofautitofauti huchukua nafasi ya kwanza kisha hufuatwa na nusu irabu, nafasi ya mwisho huchukuliwa na irabu kwa mfano;

b\$wε\$ka

p\$wa\$gu

m\$wε\$zi

iv. Muundo wa konsonanti konsonanti nusu irabu irabu K\$K\$I\$%I\$I

Ni muhimu tutaje kwamba sio maneno mengi katika lugha ya Kiswahili huundwa kwa njia hii. Mara nyingi katika muundo huu wa silabi, nafasi ya kwanza huchukuliwa na konsonanti ya nazali, kisha inafuatwa na konsonanti hasa kipasuo, kasha nusu irabu ambayo huwa na nafasi ya mwisho huchukuliwa na irabu.

Kwa mfano:

a\$n\$ \$wa

m\$b\$ εw\$ha

v. **Muundo wa irabu pekee I**

Muundo huu huwa na irabu moja; mara nyingi hutokea katika nafasi yoyote ya neno. Kwa mfano;

u\$a

o\$a

vi. **Muundo wa konsonanti pekee**

Kulingana na utafiti uliofanywa ni nazali tu ambazo hutumika katika muundo huu, hata hivyo sio nazali zote. Hali hii hujitokeza katika maneno fulani wala sio yote. Hutumika kama silabi mwanzoni mwa neno au katikati bali sio mwisho. Kwa mfano:

m\$t \$t

m\$g \$n\$ j\$wa

vii. **Muundo wa konsonanti irabu irabu K\$ISI**

Mfuatano huu wa irabu unadhihirisha irabu ndefu ambayo ndio huwa sifa bainifu tu katika jazi mlinganuo finyu. Kwa mfano:

ka:ka:

ma:fa

Muundo huu hautumiki sana katika lugha ya Kiswahili.

viii. **Silabi Funge**

